

**MAELEZO YA KATIBU WA TUME YA UTUMISHI WA UMMA WAKATI
WA KUFUNGA MAFUNZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA SHERIA YA
UTUMISHI WA UMMA [SURA YA 298, MAREJEO YA MWAKA 2019] NA
OPRAS KWA WATUMISHI WA KADCO, TAREHE 21 MEI, 2021 KATIKA
UKUMBI WA KADCO MOSHI, KILIMANJARO**

**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uendelezaji Uwanja wa
Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro KADCO,
Wawezeshaji kutoka Ofis ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,
Menejimenti ya KADCO,
Washiriki wa mafunzo,
Waandishi wa habari ,
Mabibi na mabwana;**

Ninawasalimia katika Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kutujalia uzima, nguvu na afya njema ya kutuwezesha kukutana leo kwa ajili ya shughuli ya kufunga mafunzo haya kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma [Sura ya 298, Marejeo ya mwaka 2019] na OPRAS. Nitumie fursa hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Menejimenti ya KADCO kwa kunipa heshima ya kuwa mgeni rasmi katika hafla hii muhimu.

Ndugu Washiriki;

Nimejulishwa kuwa, takribani watumishi 270 wa KADCO wa ngazi mbalimbali wamepatiwa mafunzo haya katika makundi matano (5) kwa siku mbili mbili kuanzia tarehe 10/05/2021. Pia, nimejulishwa kuwa Mada tatu ambazo ni ***Misingi ya Sheria katika Kusimamia Haki na Wajibu kwa Watumishi wa Umma, OPRAS na Majukumu ya Tume katika Usimamizi wa Rasilimali Watu*** ziliwasilishwa kwa watumishi wa kawaida na kwa upande wa Menejimenti, Mada za ***Utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma [Sura ya 298, Marejeo ya Mwaka 2019] Katika Masuala ya Ajira, Nidhamu, Rufaa na Maadili, OPRAS na Majukumu ya Tume katika Usimamizi wa Rasilimali Watu*** ziliwasilishwa.

Ndugu washiriki,

Nimejulishwa pia, maeneo yaliyotolewa ufafanuzi wa kina na Wakufunzi wetu ni pamoja na Ajira mpya; uthibitishwaji kazini au kwenye cheo; Upandishwaji vyeo; Kubadilishwa kazi/cheo (Re-categorization); Uendelezaji wa Watumishi kwa njia ya mafunzo; Tathmini ya utendaji kazi (OPRAS); Likizo mbalimbali; Uchukuaji wa hatua za nidhamu; na Maadili katika Utumishi wa Umma. Aidha, nimejulishwa kuwa mafunzo yalikuwa shirikishi na Washiriki walikuwa makini na wasikivu wakati wote wa mafunzo. Hongereni sana.

Ndugu washiriki

Ni imani yangu kuwa mafunzo haya yamewaongezea ufahamu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma [Sura 298, Marejeo ya mwaka 2019] hivyo, mtaboresha utendaji kazi wenu wa kila siku katika Uwanja wetu wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na yataongeza tija katika usimamizi wa majukumu na utoaji wa mrejesho wa utekelezaji wa majukumu hayo kwa mtumishi mmoja mmoja na Taasisi kwa ujumla na hatimaye katika ushughulikiaji wa haki na wajibu kwa watumishi wa KADCO.

Ndugu washiriki,

Moja ya eneo linaloonesha kuwa na changamoto katika kaguzi za Rasilimali Watu zinazoendeshwa na Tume ya Utumishi wa Umma ni eneo la OPRAS. Nimefarijika sana kuona kuwa pamoja na maeneo mengine, mmepata fursa ya kuelekezwa namna ya kujaza na kutekeleza OPRAS kwa mujibu wa sheria. Ni matarajio yangu kuwa baada ya mafunzo haya, sasa mtajaza OPRAS kwa kuzingatia vipindi vya ujazaji na kuwa na malengo ya utendaji kazi yaliyo “SMART” ili utendaji kazi wenu utathminiwe kiusahihi zaidi kwa lengo la kufikia malengo ya mtumishi mmoja mmoja pamoja na ya Taasisi kwa ujumla.

Ndugu washiriki,

Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma ni suala lisilo na mjadala. Hakuna Taasisi ya Umma inayoweza kufikia malengo yake kama watumishi wake kama watakuwa hawazingatii maadili. Ninatambua

kwamba wote—mmejaza na kusaini Viapo vya Maadili, hivyo, kupitia mafunzo haya, mmeelezwa umuhimu wa kuzingatia viapo hivyo na madhara ya kukiuka maadili ya Utumishi wa Umma. Nichukue fursa hii kuwasahi mzingatie hivyo Viapo vyenu vya Maadili ya Utumishi wa Umma kwa ustawi wa Taasisi na Nchi yetu kwa ujumla.

Ndugu washiriki,

Kwa kuhitimisha, ni matarajio yangu kuwa kutokana na mafunzo mliyopata, kila mmoja wetu atazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma na Sheria zilizoanzisha KADCO katika kutekeleza wajibu wake ili aweze kustahili kupata haki zake kwa ustawi wa mtumishi mmoja mmoja na KADCO kwa ujumla. Aidha, nitoe rai kwa Menejimenti ya KADCO kuendelea kuweka kipaumbele kwenye suala la mafunzo mbalimbali kwa watumishi wake ili waendane na mabadiliko ya sheria na teknolojia zinazosimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi.

BAADA YA KUSEMA HAYA, NINATAMKA KUWA MAFUNZO HAYA
YAMEFUNGWA.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA